

JE? WATU WOTE WEMA WATAOKOKA?

KUTOLEWA NA ROD RUTHERFORD

Mara nyingi tumekuwa tusikia watu wakisema “Mungu atawaokoa watu wote wema”. Hii inamaanisha kwamba watu wema katika makanisa wataokolewa. Kadhalika inamaanisha kwamba mtu yeyote ambaye si mkristo isipokuwa ni mwema ataokolewa pia. Je, watu wote wataokolewa? Biblia inasemaje?

Biblia inatufundisha ya kwamba mtu hawezi kuwa mwema kiasi cha kutosha kuokolewa kwa ajili ya wema wake. Ikiwa watu wangeweza kuokolewa kwa matendo yao mema, basi kusingekuwa na sababu ya Yesu kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Mtume Paulo anaeleza, **“kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo mtu asije akajisifu,”** Waefeso 2:8-9. Vile vile Paulo aliandika, **“kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi,”** Warumi 5:6-8.

Hata watu ambao ni wema wanaofahamu tofauti ya mema na mabaya pia nao wametenda dhambi, Biblia inasema, **“ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hata kidogo. Kwa maana tumekwisha kuwashitaki wayahudi na wayunani kwamba pia wamekuwa chini ya dhambi; kama ilivyoandikwa ya kwamba, hakuna mwenye haki hata mmoja. Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,”** Warumi 3:9, 10, 23.

Katika kitabu cha Matendo sura ya kumi tunasoma habari za mtu mmoja jina lake Kornelio. Kornelio alikuwa mtu wa dini sana, walakini alikuwa hajaokolewa. Tafadhali angalia jinsi biblia inavyosema juu ya mtu huyu mwema, **“palikuwa na Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima.”** Matendo 10:1-2. Tafadhali jua **mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa kiitalia, mtu mtauwa, mchaji wa kwamba Kornelio alikuwa akimwabudu Mungu wa kweli na aliifundisha nyumba yake yote pia kumcha Mungu.** Vile vile Kornelio alikuwa mtu wa maombi. Pia alikuwa mtu mwenye moyo mwema na mwenye huruma, kwani **“aliwapa maskini sadaka nyingi.”**

Pamoja na kuwa na imani na matendo mema Kornelio hakuokolewa, lakini aliambiwa na malaika wa Mungu, **“Sasa basi, peleka watu yafa, ukamwite Simioni, aitwaye Petro. Yeye ni mgeni wa mtu mmoja, jina lake Simoni mtengeneza ngozi, ambaye nyumba yake iko pwani; atakuambia yakupasayo kutenda,”** Matendo 10:5-6.

Je, Watu wote wema wataokolewa? Jibu ni “hapana,” kwa sababu hata watu wema wametenda dhambi na dhambi hata ikiwa moja itamtenga mtu asionekane mbinguni. Yohana aliandika, **“na ndani yake hakitaingia kamwe kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo,”** Ufu. 21:27. Njia pekee ya kuondoa dhambi ni kupitia damu ya Yesu Kristo, (Ufunuo 1:5). Hili limetendeka kwa kutii kwetu injili ya Yesu Kristo. Tunasoma katika Matendo 22:16, **“basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.”** Watu wote wema hawataokolewa. Wala watu wote wa dini hawataokolewa. Haitoshi kuwa mtu wa dini, bali mtu anapaswa awe na dini iliyokubaliwa. Yesu alisema, **“kila pando asiloli panda Baba yangu wa mbinguni litang’olewa,”** Mathayo 15:13. Pia alisema, **“si kila asemaye Bwana, Bwana, ataingia katika Ufalme wa Mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye Mbinguni,”** Mathayo 7:21.

Sio watu wote wema wataokolewa, bali ni wale walio wanyenyekevu mbele za Bwana wetu Yesu Kristo na wanaofanya mapenzi yake. **“Na ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mateso yatakayompata; naye alipokamilishwa akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii,”** Waebrania 5:8-9.

Mpendwa msomaji, Je, Umeitii injili ya Yesu Kristo? Kama bado, basi umepotea! Tafadhali mpokee Yesu Kristo leo. **“....Simama, ubatizwe, uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana,”** Mdo. 22:16.

KANISA LA KRISTO

www.kanisalakristo.com

